

22Q-Madd Al-Laazim Al-Harfiyy (Neno)

II. الحُرْفِيَّ Al-Harfiyy: (ya neno)

الْمَدُ الْلَّازِمُ الْحُرْفِيُّ Al-Madd Al-Laazim Al-Harfiyy ni madd inayopatikana katika herufi zilizokuja kwenye mwanzo wa Suwrah 29 za Qur-aan zinazoitwa: الْحُرْفُ الْمُقْطَعَةُ Al-Huruwf Al-Muqatw-twa'ah (Herufi zilizoachana) kwa maana zinatamkwa kama herufi za hijaaiyyah. Jumla ya herufi hizo ni 14 ambazo zimeundwa katika ibara kadhaa mojawapo ni:

طرق سمعك النصيحة

Baadhi ya hizi Al-Huruwf Al-Muqatw-twa'ah zimekariri zaidi ya mara moja na kuzifanya jumla kuwa ni ishirini na tisa:

الْمَصْرُوْقُ الْمَسْمُوُّ الْمَرْجُوُّ الْمَسْمُوُّ طَسَّ طَسَّ طَسَّ طَسَّ
بِسْ حَمْ حَمْ

Herufi hizi zimegawika sehemu nne:

- Isiyo na madd nayo ni الف (الف) Alif -haivutwi kabisa.
- Madd harakah mbili katika herufi za طه طه ¹
- Madd haraka mbili au nne au sita katika herufi ya ع (عين) kwa kuwa inatekelezwa kwa مُدُّ اللَّيْنِ (maddul-liyn)
- Madd harakah sita katika herufi za سَقْصُ لَكَمْ (سين - نون - قاف - صاد - لام - كاف - ميم)

Imegawanyika katika sehemu mbili:

¹ Rejea mlango wa Maddutw-twabiy'iy - Alifaatu-Hayyin-Twahur

الْمَدُ الْلَّازِمُ الْحُرْفِيُّ الْمُشَقَّلُ - Al-Madd Al-Laazim Al-Harfiyy Al-Muthaqqal

Na:

الْمَدُ الْلَّازِمُ الْحُرْفِيُّ الْمُخَفَّفُ - Al-Madd Al-Laazim Al-Harfiyy Al-Mukhaffaf